Kanisa Ni Nini?

(What Is The Church?)

Na

Ellis P. Forsman

Kanisa Ni Nini?

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 17, 2011

Kanisa Ni Nini?

Mat. 16:18

Mat. 16:18, "*Nami nakwambia wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu wala milango ya kuzimu haitalishinda.*"

Yawezekana hakuna jina lingine la kidini ambalo hutumika, na kulingana mkanganyiko mkubwa uliopo miongoni mwa wanadaamu leo, kuliko neno "kanisa."

Tunasikia mengi leo kuhusu "kanisa langu", "kanisa la mke wangu", "kanisa lenu", kwamba maelezo kama hayo yamesababisha watu walichukue kanisa kutokuwa takatifu, hakuna utakaso, na hakuna umuhimu kuliko sehemu za kunywea pombe au nyumba ya kulala wageni.

Lakini, kwa nini wanadamu wasielewe na kutumia vibaya jina na kazi ya kanisa la Bwana?

Biblia kwa uwazi linatumia neno; linaonekana zaidi ya mara 100 katika Agano Jipya.

Inatumiwa kwa usafi huo na uwazi kwamba hakuna sababu ya kuwa na mkanganyiko miongoni mwa wale wanaoheshimu Neno la Mungu.

Kanisa La Biblia Siyo:

Dhehebu.

Kwa sababu ilikuwapo miaka mia kabla ya dhehebu lolote kuundwa.

- 1 Kor. 1:10-13, "*Basi ndugu zangu nawasihi, kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoj wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja. Kwa maana ndugu zangu nimearifiwa habari zenu na wale walio wa nyumbani mwa Kloe, ya kwamba iko fitina kwenu. Basi maana yangu ni hii, ya kwamba kila mtu wa kwenu kusema, mimi ni wa Paulo, na mimi ni wa Apolo, na mimi ni wa Kefa, na mimi ni wa Kristo. Je Kristo amegawanyika? Je Paulo alisulubishwa kwa ajili yenu? Au je mlibatizwa kwa jina la Paulo?*"

- 1 Kor. 3:4-10, "*Maana hapo mtu mmoja asemapo, mimi ni wa Paulo; na mwingine mimi ni wa Apolo, je ninyi si wanadamu? Basi Apolo ni nani? Na Paulo ni nani? Ni wahudumu ambao kwao mliamini; na kila mtu kama Bwana alivyompa. Mimi nilipanda, Apolo akatia maji, bali mwenye kukuza ni Mungu. Hivyo apandaye si kitu, wala atiaye*

maji, bali Mungu akuzaye. Basi yeye apandaye, na yeye atiaye maji ni wamoja, lakini kila mtu atapata thawabu yake mwenyewe sawasawa na taabu yake mwenyewe. Maana sisi tu wafanya kazi pamoja na Mungu; ninyi ni shamba la Mungu, ni jingo la Mungu. Kwa kadiri ya neema ya Mungu niliyopewa, mimi kama mkuu wa wajenzi mwenye hekima, naliuweka msingi, na mtu mwingine anajenga juu yake. Lakini kila mtu na aangalie jinsi anavyojenga juu yake."

- 1 Kor. 3:22-23, "*Kwamba ni Paulo au Apolo, au Kefa; au dunia, au uzima, au mauti; au vile vilivyopo sasa, au vile vitakavyokuwapo; vyote ni vyenu; nanyi ni wa Kristo, na Kristo ni wa Mungu.*"

Nyumba ya kimwili au jingo.

Mdo. 17:24, "*Mungu aliyeufanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo, yeye kwa kuwa ni Bwana wa mbingu na nchi, hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mikono;*"

Ni jingo la kiroho.

1 Pet. 2:5, "*Ninyi nanyi kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe nyumba ya Roho, ukuhani mtakatifu, mtoe dhabihu za roho, zinazokubaliwa na Mungu, kwa njia ya Yesu Kristo.*"

Kanisa Ni Nini?

Walioitwa. ("*Ekklesia*")

Tumeitwa na injili.

2 Thes. 2:14, "*Aliyowaitia ninyi kwa injili yetu, ili kuupata utukufu wa Bwana wetu Yesu Kristo.*"

Tumeitwa kutoka duniani, toka gizani, kuingia nuruni.

- Mdo. 26:18, "*Uwafumbue macho yao, na kuwageuza waiache giza na kuielekea nuru, waziache na nguvu za shetani na kumwelekea Mungu; kisha wapate msamaha wa dhambi zao, na uruthi miongoni mwao waliotakaswa kwa imani iliyo kwangu mimi.*"

- Kol. 1:13-14, "*Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake; ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani msamaha wa dhambi;*"

Walio okolewa.

Mdo. 2:47, "*Wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.*"

Wokovu uko ndani ya Kristo. 2 Tim. 2:10, "*Kwa ajili ya hilo nastahimili mambo yote, kwa ajili ya wateule ili wao nao waupate wokovu ule ulio katika Kristo Yesu, pamoja na utukufu wa milele.*"

Lakini mtu hawezi kuwa ndani ya Kristo bila kuwa ndani ya kanisa lake.

Tunabatizwa katika Kristo. Gal. 3:27, "*Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo.*"

Pia tunabatizwa katika mwili wake. 1 Kor. 12:13, "*Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani; ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru; nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja.*"

Mwili ndiyo kanisa.

- Kol. 1:18, "*Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtaangulizi katika yote.*"
- Efe. 1:22-23, "*Akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo ndilo mwili wake, ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote.*"

Kwa vile, kuwa ndani ya Kristo ni sawa na kuwa kaatika mwili wake, au katika kanisa lake.

Hakuna kitu kama mtu ameokolewa alafu baadae akafanyika mshirika wa kanisa.

Wale wasemao kwamba mtu anaweza kuokolewa nje ya kanisa, hawafahamu kanisa ni nini.

Waliotakaswa.

1 Kor. 1:2, "*Kwa kanisa la Mungu lililoko Korintho, wale waliotakaswa katika Kristo Yesu, walioitwa wawe watakaatifu, pamoja na wote wanaoliitia jina la Bwana wetu Yesu Kristo kila mahali, Bwana wao na wetu.*"

Kutakaswa inamanisha kuwekwa wakfu.

Kila Mkristo hutakaswa, au huwekwa wakfu, anapoitii injili ya Kristo.

- Yohana 17:17, "*Uwatakase kwa ile kweli; neno lako ndiyo kweli.*"
- Heb. 2:11, "*Maana yeye atakasaye na hao wanaotakaswa wote pia watoka kwa mmoja. Kwa ajili hii haoni haya kuwaita ndugu zake;*"

Wakorintho walitakaswa, au waliwekwa wakfu.

1 Kor. 6:9-11, "*Au hamjui ya kuwa wadhaalimu hawatauridhi ufalme wa Mungu? Msidanganyike; waasherati hawataurithi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti, wala wevi, wala watamanio, wala walevi, wala watukanaji, wala wanyang'anyi. Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii; lakini mlioshwa, laikini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu.*"

Kuna Matamshi Kadhaa Zipatikanazo Katika Agano Jipya Ikielezea Kanisa

Mwili wa Kristo.

1 Kor. 12:27, "*Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila mmoja peke yake.*"

Kanisa la Kristo.

Rom. 16:16, "*Salimianeni kwa busu takatifu. Makanisa yote ya Kristo yawasalimu.*"

Kanisa la Mungu.

- 1 Kor. 1:2, "*Kwa kanisa la Mungu lililoko Korintho, wale waliotakaswa katika Kristo Yesu, walioitwa wawe watakaatifu, pamoja na wote wanaoliitia jina la Bwana wetu Yesu Kristo kila mahali, Bwana wao na wetu.*"
- Mdo. 20:28, "*Jitunzeni nafsi zenu na lile kundi lote nalo ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe.*"

Bibi harusi wa Kristo.

Kanisa ni bibi harusi wa Kristo. "*Enyi wake watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu. Kwa maana mume ni kichwa chaa mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha kanisa; naye ni mwokozi wa mwili. Lakini kama vile Kanisa limtiivyo Kristo vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo. Enyi waume wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa,akajitoa kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno; apate kujiletea Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lolote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa. Vivyo hivyo imewapasa waume nao kuwapenda wake zao kama*

miili yao wenyewe. Ampendaye mkewe hujipenda mwenyewe. Maana hakuna anayeuchukia mwili wake popote; bali huulisha na kuutunza, kama Kristo naye anavyolitendea kanisa. Kwa kuwa tu viungo vya mwili wake. Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja. Siri hiyo ni kubwa ila mimi nanena haabari ya Kristo na Kanisa." (Efe. 5:22-32).

Je kwa mtazamo wako unaona kwamba katika ndoa kati ya mume na mke mwanamke anapaswa kuvaa au kutumia jina la mtu mwingine? Mwanamume ye yote anaweza kuchukia kama mkewe anatumia jina la mwingine. Je ulikuwa unafahamu kwamba tendo la mke kutumia jina la mumewe linarudi nyuma kwa Adamu na Eva? "*Mwanamume na mwanamke aliwaumba, akawabariki akawaita jina lao Adamu, siku ile walipoumbwa.*" (Mwa. 5:2). Kila mmoja Mungu aliwaita Adamu na Eva, lakini kaama wenza walioana, Mungu aliwaita Adamu.

Kanisa la mzao wa kwanza.

Heb. 12:23, "*Mkutano mkuu na kanisa la wazaliwa wa kwanza walioandikwa mbinguni, na Mungu mwamuzi wa watu wote, na roho za watu wenye haki waliokamilika,*"

Hatupaswi kutumia jina lingine.

Mdo. 4:10-12, "*Jueni ninyi nyote na watu wote wa Israeli ya kuwa kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, ambaye ninyi mlimsulubisha, na Mungu akamfufua katika wafu, kwa jina hilo mtu huyu anasimama ali mzima mbele yenu. Yeye ndiye jiwe lile lililodharauliwa na ninyi waashi, nalo limewekwa kuwa jiwe kuu la pembeni. Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.*"

Neno "Kanisa" Linatumiwa Katika Agano Jipya Katika Mitazamo Miwili

Katika mtazamo wa jumla.

Mat. 16:18, "*Nami nakwambia wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu wala milango ya kuzimu haitalishinda.*"

Katika mtazamo wa umoja.

- 1 Kor. 1:2, "*Kwa kanisa la Mungu lililoko Korintho, wale waliotakaswa katika Kristo Yesu, walioitwa wawe watakaatifu,*

pamoja na wote wanaoliitia jina la Bwana wetu Yesu Kristo kila mahali, Bwana wao na wetu."

- 1 Thes. 1:1, "*Paulo na Silwano, na Timotheo kwa kanisa la Wathesalonike, lililo katika Mungu Baba, na katika Bwana Yesu Kristo. Neema na iwe kwenu na amani.*"

Neno "kusanyiko" linatokana na maneno mawili ya Kilatini, "con", ikimanisha "na" au "pamoja", au "grex", ikimanisha "kundi".

Hitimisho

Kanisa ni nini? Hakika tumeweza kuona kwamba kanisa linaundwa na watu walio okolewa; katika mtazamo wa jumla, inajumuisha waongofu wote wa ulimwenguni, na katika mtazamo wa umoja, inajumuisha Wakristo wote katika kusanyiko.

Mtu anawezaje kuwa mshiriki wa kanisa la Kristo? Lazima afanyike Mkristo. Zifuatazo ni hatua muhimu zinazofanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Waeb. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa dhawabu wale wamtafutao.*" Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na mimi akniambia kwamba haamini kwamba Mungu yuko. Kwa vile nilisha batizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye kuhusu mandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya ukristo ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamba Mungu yuko. Lakini ili kuwa upande salama, labda anapaswa kwenda kanisani, na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kuwa amekwenda kanisani atampeleka mbinguni (kama kuna mbingu), na si motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "haifanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima uamini katika yeye kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza.

- **Toba.** Matend. 2:38, "*Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*" Matend 11:18, "*...Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao <u>toba liletalo uzima</u>.*" Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, "Kwamba kuna mwizi!" taratibu unachukua simu ya mkononi, unawapigia polisi. Kidogo polisi wanafika na kumshika mwizi. Alafu anapiga kelele, "samahani; samahani!" Anaomba msamaha wa nini? Kwa sababu

amekamatwa; si kwamba ameiba. Toba iliyokweli ni kwamba mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena. Hiyo ndio toba ya kweli. Ni badiliko la nia linaloleta badiliko la matendo. Tunatakiwa kufanya hivyo kabla hatujawa wakristo.

- **Kukiri.** Waru. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*"

  Tuna kiri nini? Kwamba tuna amini kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu.

  Kumbuka kwamba katika andiko hilo hapo juu kwamba imani (kuamini), toba, na kukiri ni "KATIKA" haki, uzima, au wokovu. "Katika" inamanisha kuelekeza kwenye kitu Fulani; si kwamba mtu ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu mwenyewe alibatizwa kuitimiza haki yote, "*Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa, kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, huyu ni mwanangu mpendwa, ninaye pendezwa naye.*" (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo sahihi la kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema, "*Imekuwa kwetu **sisi** kuitimiza haki yote.*" Tuna batizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, si kwa sababu ni haki yetu.

  Kwa kweli, tusipo batizwa, tungali katika dhambi zetu. "*Petro kawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu*" (Matend. 2:38). *Petro, umesema kusudi la ubatizo ni nini?*" *Kwa ajili ya ondoleo la dhambi*". Kwa nini watu wanapenda kuach hatua inayotuondoa dhambi zetu

  Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu lazima tubatizwe. "*Na akawambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*" (Marko 16:15-16).

  Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu iki hiki, "*Unakawilia nini? Simama, na ubatizwe, na uoshwe dhambi zako,*

ukiliitia jina la Bwana." (Matend. 22:16). Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko, "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*" (Waru. 6:4). Utu wetu wa kale umekufa. "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake. Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlvyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika katika mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusiitumikie dhambi tena.*" (Waru. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu inayotumiwa na damu ya Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tunakuwa huru na dhambi zetu za zamani kama tu tukibatizwa.

Hii haimanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatuwezi kupeleka maiti makaburini, na kumwekea udongo kidogo juu yake; tunauzika mwili.

Kama hujafanyika Mkristo, kwa nini usifanyike?